Endorsed by GEEAP
Global Education Evidence Advisory Panel

Mbinu Madhubuti za Kufundisha Kusoma katika Nchi za Kipato cha Chini na cha Kati: Ushahidi Unaonyesha Nini

Muhtasari mkuu

Kujifunza kusoma ni muhimu kwa hadhi, uhuru na maendeleo ya binadamu. Kujua kusoma na kuandika ndio msingi wa masomo yote na niyamaana kuongeza nafasi mbalimbali maishani kwa kiasi kikubwa. Kwenye ngazi ya kitaifa, nchi ambazo zina viwango vya juu vya ujuzi wa kusoma na kuandika huimarika pakubwa kiuchumi, huwa na upungufu wa matukio ya ukosefu wa usawa na huboresha matokeo ya afya ya umma. Kwenye ngazi ya kibinafsi, wanafunzi wanaosoma vizuri wana uwezekano mkubwa wa kufaulu katika masomo yote shuleni, huku wanafunzi wasiojifunza kusoma wanapata manufaa machache ya kielimu na kikazi na mapato ya chini maishani. Zaidi ya hayo, iwapo watoto hawawezi kusoma , uwekezaji katika maeneo mengine ya elimu hakutimizi matokeo yanayotarajiwa. Kuhakikisha kuwa watoto wote wanajifunza kusoma wajibu wa uadilifu na hitaji la kiuchumi kwa kila taifa.

Kwa bahati mbaya, watoto wengi katika nchi za mapato ya chini na ya kati (LMIC, low and middle-income countries) hawajifunzi kusoma. Kufikia umri wa miaka kumi, asilimia sabini (70%) ya watoto katika nchi za mapato ya chini na ya kati (LMIC) hawawezi kusoma na kuelewa maandishi rahisi ya kiwango cha umri wao. Katika nchi nyingi, baada ya kujifunza kwa miaka kadhaa, watoto hawajakaribia ustadi unaotarajiwa, wana uwezekano mdogo sana wa kuwa wasomaji. Hata hivyo, kuna ushahidi wa kutosha kuwa kuboresha mafunzo ya kusoma kunaweza kuongeza pakubwa viwango vya kusoma.

This report was produced by a group of literacy experts and is endorsed by the Global Education Evidence Advisory Panel (GEEAP). The Panel is convened by the Foreign, Commonwealth & Development Office (FCDO), The World Bank, and the United Nations Children's Fund (UNICEF).

Foreign, Commonwealth & Development Office
THE WORLD BANK IBRD • IDA | WORLD BANK GROUP
unicef for every child

Mojawapo ya sababu za msingi za tatizo hili la kutokusoma na kutokuandika ni kukosa kutumia mbinu za mafunzo zilizothibitishwa kwa utafiti. Mifumo mingi ya elimu inaendelea kutumia njia zilizopitwa na wakati ambazo utafiti umeonyesha kuwa hazifai au hazina mwongozo wazi kuhusu jinsi ya kufunza kusoma kwa ufanisi. Vipengele vingi ambavyo huchangia matokeo mabaya ya kusoma ni pamoja na uhaba wa vitabu, mafunzo duni ya yasiyo ya kutosha ya walimu na mafunzo endelevu ya kitaaluma, utoro wa kiwango cha juu, muda mfupi darasani, mafunzo katika lugha zisiyofahamika na mafunzo ambayo hayalingani na viwango vya masomo vya watoto—yote haya yakichangiwa na ukosefu mkubwa wa kutumia mbinu za kusoma za kisayansi.

Kwa bahati nzuri, utafiti wa kisayansi sasa unatoa mwongozo wazi kuhusu jinsi watoto hujifunza kusoma na jinsi ya kuwafundisha kwa ufanisi. Kusoma ni mojawapo ya maeneo yaliyofanyiwa utafiti sana ya mafunzo ya binadamu, kwa utafiti wa zaidi ya karne moja. Ingawa utafiti wa zamani ulilenga tu nchi zinazozungumza Kiingereza na za mapato ya juu, msingi wa utafiti umeongezeka pakubwa. Ripoti hii inajumuisha utafiti endelevu kutoka nchi za LMIC, ikikagua zaidi ya tafiti 151 kuhusu mafunzo ya kusoma yanayofaa yaliyofanyika kote Afrika, Asia, Amerika ya Kusini, Karibiani, na Mashariki ya Kati zikitumia zaidi ya lugha 167 tofauti tofauti. Ushahidi huu mpana unathibitisha kuwa kanuni fulani za msingi za mafunzo ya kusoma yanayofaa ni za jumla, ingawa vipengele mahususi vya mafunzo vinaweza kutumiwa katika lugha, mifumo ya uandishi na miktadha ya utamaduni mbalimbali.

Utafiti huu unaonyesha kuwa kusoma kwa ufahamu ni mchakato tata unaotegemea ujuzi mwingi unaohusiana. Ujuzi huu unaweza kuainishwa katika nyanja mbili pana: **usimbuaji na ufahamu wa lugha.** *Usimbuaji* ni uwezo wa kutambua ishara zilizoandikwa (k.m, herufi) na kuzibadilisha kuwa sauti zinazowakilisha ili kutambua maneno. Ufahamu wa lugha huhusisha kuelewa maana halisi ya maneno, sentensi na maandiko. Ujuzi wa usimbuaji na ufahamu wa lugha ni muhimu na huambatana wakati watoto wanasoma: bila ujuzi wa kusimbua, watoto hawawezi kutambua maneno; bila ufahamu wa lugha, hawawezi kuelewa maana yake (Gough & Tunmer, 1986). Mafunzo faafu ya kusoma lazima yakuze maeneo yote ya ujuzi kwa pamoja. Misingi hii huanza katika miaka ya utotoni, nyumbani au katika masomo rasmi ya mapema ya watoto na kuwa lengo la madarasa ya msingi.

Ili kukuza uwezo huu muhimu wa kusoma, watoto wanahitaji mafunzo ya hatua kwa hatua a na ya kimfumo katika maeneo sita muhimu:

1. **Ukuaji wa lugha ya matamshi:** hii inajumuisha ujuzi wa kusikiliza na kuzungumza na kukuza msamiati. Lazima watoto waelewe maneno yanayotamkwa kabla ya kuelewa maandishi yaliyoandikwa. Ingawa watoto kwa kawaida huimarisha baadhi ya ujuzi wa lugha ya matamshi, mafunzo lengwa ya darasani huharakisha pakubwa ukuaji huu.
2. **Ufahamu wa kifonolojia:** huu ni uwezo wa kutambua na kutumia sauti mahususi katika lugha ya mazungumzo. Lazima watoto waelewe kuwa maneno yanayozungumzwa hutokana na vitengo vidogo vya sauti kabla ya kuunganisha herufi kwenye sauti hizo na kuzichanganya kuwa maneno.
3. **Mafunzo ya foniki ya kimfumo:** hii inarejelea kuwafunza watoto uhusiano mahususi kati ya herufi na sauti na jinsi ya kuziunganisha ili kutengeneza maneno. Watoto hujifunza “kusema kwa sauti” maneno wasiyoyafahamu kwa kutambua kila sauti ya herufi na kuziweka pamoja.
4. **Ufasaha wa kusoma:** huu ni uwezo wa kusoma maandishi kwa usahihi, haraka na njia inayofaa. Ufasaha wa kusoma hufungua uwezo wa akili ili kuelewa maana badala ya kupambana kutambua maneno mahususi.
5. **Ufahamu wa kusoma:** :kama sehemu ya mafunzo ya kusoma, watoto pia hunufaika kutokana na mafunzo dhahiri katika mbinu maalum za kuelewa maandishi, kama vile kufuatilia ufahamu wao wenyewe na kukuza maarifa kuhusu ulimwengu.

6. **Kuandika:** msingi thabiti wa ushahidi, ikijumuisha utafiti unaoibuka kutoka kwa nchi za LMIC, unaonyesha kuwa mafunzo ya kuandika—yakiwemo kubuni herufi, tahajia, na kutunga maandiko—husaidia kabisa ukuaji wa kusoma na kuimarisha ujuzi mwingine muhimu.

Stadi hizi sita lazima zifunzwe kwa njia dhahiri, hatua kwa hatua na kwa kina. *Mafunzo dhahiri* inamaanisha kuwa walimu wanaonyesha moja kwa moja na kueleza kila ujuzi, wakitoa mifano wazi kabla ya wanafunzi kufanya mazoezi kwa kujitegemea. *Mafunzo ya hatua kwa hatua* humaanisha kuwa stadi hufunzwa kwa mpangilio wa kimantiki, ukifuata upeo na mfululizo uliopangwa. *Mafunzo ya kina* humaanisha kushughulikia maeneo yote sita ya stadi, kwa kuwa udhaifu katika eneo lolote unaweza kuwazuia watoto kuwa wasomaji wema. Mtazamo huu unatofautiana na mbinu ambazo huwatarajia watoto kugundua ujuzi wa kusoma kivyao au zile ambazo hulenga vipengele fulani tu vya kusoma.

Maarifa ya kimsingi kutoka kwa utafiti wa kusoma ni kuwa watoto hawajifunzi kusoma kwa kiasili—kusoma kunapaswa kufunzwa kwa njia dhahiri. Tofauti na lugha inayozungumzwa, ambayo watoto hupata kwa njia ya kiasili kupitia mafichuo kwa mazingira, kusoma huhitaji mafunzo ya moja kwa moja. Ushahidi kutoka kwa nyurosayansi na saikolojia ya utambuzi huonyesha kuwa wasomaji wenye ujuzi huchakata maneno kwa kuunganisha herufi haraka na sauti zake husika, badala ya kujaribu kukumbuka meneno mazima au kukisia maana kutoka kwa muktadha. Kuelewa huku kwa kisayansi kunathibitisha kuwa watoto wanahitaji mafunzo dhahiri, ya hatua kwa hatua kuhusu jinsi herufi huwakilisha sauti na jinsi ya kuunganisha sauti hizi kuwa maneno.

Kanuni za msingi za mafunzo ya kusoma yanayofaa ni za jumla, lakini mipango fanisi hubadilisha vigezo fulani vya mafunzo kuzingatia makala ya lugha na mahitaji mahususi ya mwanafunzi. Kwanza, watoto walio katika darasa moja mara kwa mara huwa na uwezo tofauti wa kusoma. Lazima masomo yapangwe ili kuwashughulikia wanafunzi katika ngazi zao za sasa za kujifunza, ili kuhakikisha kuwa wasomaji wanaotatizika wanapokea usaidizi wa kimsingi kabla ya kuendelea katika ujuzi wa juu. Kwa wale wanaotatizika, marekebisho mahususi yanaweza kujumuisha usaidizi wa mwanafunzi binafsi au kikundi kidogo, mbinu za hisia nyingi na nyenzo za mafunzo zinazofikiwa. Pili, lugha tofauti huhitaji mbinu tofauti za mafunzo. Kwa mfano, ingawa mafunzo ya foniki za kimfumo ni ya manufaa katika alfabeti na lugha za kialfabeti, kuna tofauti fulani katika kiwango cha mafunzo ya foniki yanayohitajika. Lugha zilizo na mitindo thabiti zaidi ya tahajia (kama vile Kiswahili na Kihispania) huhitaji muda mfupi wa mafunzo ya uhusiano wa herufi na sauti kuliko lugha zilizo na tahajia changamano zisizo za kawaida (kama vile Kiingereza na Kifaransa). Vilevile, mifumo ya uandishi wa alfasilabiki kama vile Kidevanagari, Kikanada na Kitamili hutumia idadi kubwa zaidi ya ishara na huhitaji mafunzo mengi zaidi ili kufahamu ishara.

Kanuni tatu za ziada ambazo ni muhimu kwa mafunzo ya kusoma kwa ufanisi.

Kwanza, lugha ya mafunzo huathiri pakubwa kuimarika kwa watoto katika kusoma. Zaidi ya theluthi moja ya watoto, katika nchi za LMIC hufunzwa kusoma katika lugha ambayo hawaizungumzi au kuielewa vyema. Hali hii huweka vizuizi vikuu katika uwezo wa kusoma na kuandika, na kusababisha maendeleo ya polepole na ufasaha wa chini katika kusoma. Mara kwa mara, utafiti huonyesha kuwa watoto hujifunza kusoma kwa ufanisi zaidi wanapofunzwa kwanza katika lugha yao ya nyumbani. Wakati ambapo huwezi kutumia lugha ya nyumbani kwa mafunzo, watoto huhitaji muda mwingi zaidi na usaidizi wa ndani ili kukuza ujuzi wa kuzungumza katika lugha ya mafunzo kabla ya kuweza kusoma kwa ufanisi katika lugha hiyo. Watunzi wa sera wanapaswa kutathmini kwa makini muktadha wa lugha za nchi yao kabla ya kuamua sera za lugha ya mafunzo.

Pili, ubora wa utekelezaji ni muhimu kwa ufanisi wa mpango. Hata mipango bora ya kusoma inaweza kufeli isipotekelezwa inavyofaa. Ufanisi huhitaji kuendana na vipaumbele vya mifumo iliyopo ya serikali; kuhakikisha miundo endelevu inayoweza kustahimili ufadhili wa mwanzo; kuwasaidia walimu katika kuasilisha mbinu mpya; kubuni nyenzo za kufunza na kujifunza zilizo rahisi kutumia; na kujumuisha maudhui husika katika mafunzo ya

awali ya ualimu yanayozingatia ujuzi na maendeleo ya kitaaluma. Lazima mipango ifuatilie mara kwa mara jinsi walimu wanavyotekeleza mbinu mpya na kutoa maoni ya haraka ili kufanya marekebisho yanayohitajika.

Tatu, mafunzo ya kusoma yanayozingatia ushahidi yanaweza kuwa ya nafuu zaidi kuliko njia mbadala. Kuwekeza katika mbinu zilizothibitishwa za kusoma katika miaka ya mapema ya shule ya watoto kunaweza kupunguza hitaji la mipango ghali ya kurekebisha baadaye, kupunguza kurudia kwa darasa na kupunguza idadi ya viwango vya kuacha shule. Mipango ya pedagojia inayojumuisha mafunzo ya kusoma yanayozingatia ushahidi wa utafiti ni miongoni mwa mikakati ya kielimu ya gharama ya chini zaidi inayopatikana. Hii hufanya mafunzo ya kusoma yanayozingatia ushahidi wa utafiti kuvutia hasa kwa nchi zinazotarajia matokeo ya kiwango cha juu kutoka kwa bajeti za chini za kielimu.

Tunawasihi watunzi wa sera za elimu kuendeleza mafunzo yanayozingatia ushahidi wa utafiti ili watoto wengi wawe wasomaji wenye ustadi. Uboreshaji mkubwa katika matokeo ya kusoma hauawezekani tu ila pia unaweza kutimizwa katika muda unaofaa. Uboreshaji kama huo ni muhimu kwa maendeleo ya kielimu, ukuaji wa kiuchumi na maendeleo ya kijamii. Kulingana na ushahidi wa utafiti mpana uliowasilishwa katika ripoti hii, tunapendekeza watunzi wa sera:

1. **Kuweka ahadi ya kitaifa** ili kuhakikisha kuwa watoto wote wanakuwa wasomaji bora kupitia mafunzo yanayozingatia ushahidi wa utafiti unaofaa.
2. **Kuchagua lugha ya mafunzo inayofaa** na kuwapa watoto usaidizi wanaohitaji ili kujifunza kusoma katika lugha hizo.
3. **Kuwasilisha mafunzo ya kusoma yaliyo dhahiri, ya hatua kwa hatua na ya kina katika stadi zote sita muhimu**: lugha ya matamshi, ufahamu wa kifonolojia, foniki za kimfumo, ufasaha wa kusoma, kufahamu kusoma na kuandika. Kuhakikisha kuwa mafunzo ni dhahiri na ya hatua kwa hatua—bila kuwaacha watoto 'kujaribu kuelewa wenyewe'. Kuwapa wanafunzi muda wa kutosha kwa kufanya mazoezi ya kusoma—ikijumuisha fursa nzuri za kujihusisha na vitabu, kusoma makala mbalimbali kivyao na kubuni mazoea ya kusoma.
4. **Kuasilisha mafunzo kuzingatia sifa za lugha:** kanuni za msingi za mafunzo ya kusoma yanayolingana na ushahidi wa utafiti ni za jumla, lakini mipango fanisi hufanya mafunzo kushughulikia mahitaji ya kimktadha.
5. **Kulenga utekelezaji unaofaa** kwa kuwapa walimu usaidizi bora, nyenzo zilizo rahisi kutumia na mafunzo endelevu ya kitaaluma.

Mbinu hizi zinazozingatia ushahidi lazima ziasilishwe kwa umakini kulingana na muktadha wa nchi mahususi, lugha, utamaduni na elimu huku zikidumisha usahihi wa kanuni muhimu ambazo utafiti umethibitisha kuwa zinafaa.

Access the full paper here: **GEEAP.org**

Authors: The research, analysis and writing of this forthcoming paper was done by (in alphabetical order by last name): Horacio Alvarez-Marinelli, Izzy Boggild-Jones, Michael Crawford, Margaret "Peggy" Dubeck, Dhir Jhingran, Christopher Lack, Nompumelelo Mohohlwane, Maria Eugenia Oviedo, Benjamin Piper, Jaime Saavedra, Hanada Taha.

The paper was written by a multidisciplinary team and developed and led by recognized experts in literacy, with guidance from GEEAP panel members with relevant expertise. The broader GEEAP panel reviewed aspects of the research methodology, the peer-review process, and the quality standards, and provided comments and suggestions that were addressed by the authors.

The judgments are the authors' own, drawing on their reading of the available research and evidence. Thus, their conclusions do not necessarily reflect the policy positions of the Panelists, the Panelists' institutions, or of the GEEAP convening institutions.